OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

30/06/2025 ► 05/07/2025

OAG

HABARI KITAIFA

# Ofisi AG yatambua ushirikiano kwenye vyombo vya habari

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno, amekutana na kufanya mazungumzo na ujumbe kutoka Kampuni ya The Guardian Limited, wachapishaji wa magazeti ya The Guardian na Nipashe, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma, Juni 26, 2025.

Katika mazungumzo hayo yaliyolenga kuimarisha uhusiano kati ya taasisi za kiserikali na vyombo vya habari pamoja na kujadiliana juu ya taasisi hizo zinavyoweza kushirikiana katika kuwahabarisha wananchi majukumu na mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa katika Sekta ya Sheria, ameeleza namna sheria za uchaguzi zimefanyiwa marekebisho.

Alisema wapo wanaosema hazijabadilishwa jambo ambalo si sahihi kwa kuwa mabadiliko yaliyofanyika ni makubwa kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unakuwa huru na haki.

**"Tangu 1994 muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), haikuwa kama ilivyo sasa ambapo kuna mchakato wa kisheria wa kuwapata wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC),**

Marekani wanaw... ka wagombea bi... afsi, tujiulize kw... mazingira ya nc... zetu tunaweza hili? Tutakuwa n... karatasi ya kupi... kura ndefu kiasi gani? Tutakuwa na wafanyakazi wangapi? Je INE... itakuwa na ukubwa kiasi gani," alisema.

Naibu Mwanasheria Mkuu w... Serikali, alisema muhimu kwa vyombo vya habar... kutoa elimu ya Sheria y... Uchaguzi kwa wananch... ili waweze kuielewa.

"Niwaombe mwendel... kutoa elimu ya sheria mbalimbali na katika ki... indi hiki tulichopo toen... elimu ya kutosha kuhus... Sheria za Uchaguzi ili w... nanchi waweze kuielewa," alisema Maneno.

Aidha, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza kuwa Ofi... yake iko tayari muda wowote kushirikiana n... vyombo vya habari ili kuweza kutoa taarifa sahihi kwa wananchi.

Alisema Ofisi ya Mwa... nasheria Mkuu wa Serikali inatambua mchang... mkubwa wa vyombo...

zimefanyiwa marekebisho.

Alisema wapo wanaosema hazijabadilishwa jambo ambalo si sahihi kwa kuwa mabadiliko yaliyofanyika ni makubwa kuhakikisha mchakato wa uchaguzi unakuwa huru na haki.

"Tangu 1994 muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), haikuwa kama ilivyo sasa ambapo kuna mchakato wa kisheria wa kuwapata wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), ambao uko kwa uwazi na shirikishi," alisema.

Kuhusu kwanini matokeo ya Rais hayapingwi mahakamani, alisema ikiruhusiwa hivyo maana yake nchi haitakuwa na uongozi wa Rais na Makamu wa Rais kwa muda mrefu na hakuna uhakika atakayeshinda naye hatapingwa mahakamani.

Aidha, kwa mgombea binafsi alisema ikiwa kila mmoja ataruhusiwa kugombea maana yake kutakuwa na kazi kubwa kwa INEC, kuandaa karatasi za kura na usimamizi wa mchakato husika, na kwamba mazingira ya mgombea binafsi hutegemea mambo mengi kwa nchi husika.

"Tusiseme mbona

kali ameeleza kuwa Ofisi yake iko tayari muda wowote kushirikiana na vyombo vya habari ili kuweza kutoa taarifa sahihi kwa wananchi.

Alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatambua mchango mkubwa wa vyombo vya habari katika kukuza demokrasia, kutoa elimu kwa umma, na kushirikiana na taasisi za umma katika kuhimiza utawala bora. "Tunatambua nafasi ya vyombo vya habari katika kutoa elimu kwa wananchi, Ofisi yetu iko wazi muda wote kushirikiana nanyi katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi kupitia vyombo vya habari," alisema.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa The Guardian Limited, Jackson Paulo aliishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapokezi mazuri waliyoyapata na ziara yao imekuwa na mafanikio makubwa kwakuwa wamejifunza mambo mengi ya kisheria huku akiahidi wataendeleza ushirikiano huo kwa kuuhabarisha umma juu ya masuala mbalimbali ya kisheria yanayotekelezwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

# Johari apongeza mchango wa Mahakama urekebu wa sheria

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amemshukuru Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji George Masaju kwa mchango ambao mahakama imeutoa katika kufanikisha urekebu wa sheria.

Johari alitoa kauli hiyo wakati akimkabidhi Juzuu za Sheria zilizofanyiwa urekebu Toleo la Mwaka 2023, Jaji Masaju ofisini kwake jijini Dodoma juzi.

Alisema kuanza kutumika kwa sheria kutairahisishia mahakama wakati wa kutekeleza majukumu yake ya utendaji haki kwa wananchi.

"Mheshimiwa Jaji Mkuu baada ya kukamilika kwa urekebu na Rais alizindua na alitoa tamko kwamba sheria hizi zianze kutumika kuanzia Julai Mosi, hivyo tumekuja na timu yangu kuja kukukabidhi rasmi juzuu hizi zilizofanyiwa urekebu," alisema Johari.

Aidha, alieleza kuwa

urekebu," alisema Johari.
Aidha, alieleza kuwa

mradi wa urekebu wa sheria umefanyika kwa kutumia rasilimali za fedha za ndani na rasilimaliwatu wa ndani, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambako mradi huo ulikuwa ukiendeshwa na wahisani.

"Kitu kizuri ni kwamba huu mradi tumeufanya kwa fedha zetu za ndani na hata publisher (mchapishaji) ni wa ndani, kuanzia sasa hatutasubiri tena miaka 10 zile annual supplement (nyongeza za kila mwaka) sasa tutahakikisha tunazitoa ipasavyo ili ikifika miaka 10 mradi usiwe mkubwa sana," alieleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Akipokea juzuu hizo, Jaji Masaju aliishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutambua mchango wa mahakama katika kufanikisha kazi hiyo, na kueleza kuwa mahakama ni mtumiaji mkubwa wa sheria hizo na zitasaidia katika utendaji kazi wao.

"Sisi kama mahakama ni moja ya watumiaji wakuu kwa sababu mambo mengi yanaishia mahakamani hivyo tukiwa na hizi juzuu zitatusaidia sana," alisema Jaji Mkuu.

Katika hatua nyingine, aliipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuukamilisha mradi wa urekebu wa sheria kwa kutumia rasimali fedha za ndani pamoja na kuzifanya sheria hizo kupatikana bure kwa njia ya mtandao na kuwasaidia watumiaji wengi kuzipata kwa urahisi.

Awali, Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole alimpongeza Jaji Mkuu wa Tanzania kwa mchango wake katika kukamilisha kazi hiyo tangu akiwa Mwanasheria Mkuu

kamilisha kazi hiyo tangu
akiwa Mwanasheria Mkuu

wa Serikali, ambapo alisema wamekabidhi seti ya juzuu za sheria za nchi 20 ambayo ina jumla ya sheria kuu 446.

Vilevile, alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetekeleza maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha sheria hizo zinapatikana, na kwa sasa zinapatikana katika mfumo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujulikanao kama OAG-MIS.

Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu Toleo la Mwaka 2023 zilisainiwa na kutolewa tamko na Rais Samia Suluhu Hassan Aprili 23, mwaka huu na zimeanza kutumika kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Habari

# Mwanasheria Mkuu wa Serikali amkabidhi Jaji Mkuu juzuu za sheria zilizofanyiwa urekebu



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amemkabidhi Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la Mwaka 2023 Jaji Mkuu wa Tanzania Jaji George Masaju Ofisini kwake Jijini Dodoma Julai 03, 2025.

Akizungumza wakati wa kukabidhi Juzuu hizo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amemshukuru Jaji Mkuu kwa mchango ambao Mahakama umeutoa katika kufanikisha zoezi la Urekebu wa Sheria ambapo ameeleza kuanza kutumika kwa sheria kutairahisishia Mahakama wakati wa kutekeleza majukumu yake ya utendaji haki kwa wananchi.

"Jaji Mkuu baada ya kukamilika kwa zoezi la urekebu na Rais alizindua na alitoa tamko kwamba Sheria hizi zianze kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, hivyo tumekuja na timu yangu kuja kukukabidhi rasmi Juzuu hizi zilizofanyiwa Urekebu." Amesema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza kuwa mradi wa urekebu wa sheria umefanyika kwa kutumia rasilimali za fedha za ndani na rasilimali watu wa ndani, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo mradi huo ulikuwa ukiendeshwa na Wahisani.

# Revised Laws officially handed over to Judiciary to enhance access to Justice

by THE RESPONDENT ONLINE - July 04, 2025

Advertisement



**By Our Correspondent Reporter**

The Attorney General of Tanzania, Hamza S. Johari, has officially handed over the 2023 Edition of the Revised Laws of Tanzania to the Chief Justice, Prof. George M. Masaju, marking a significant step forward in improving access to justice and strengthening the rule of law in the country.

The handover ceremony, held on July 3, 2025, at the Chief Justice's office in Dodoma, follows the directive by President Samia Suluhu Hassan, who officially signed and declared the revised laws operational as of July 1, 2025.

Speaking at the event, the Attorney General emphasized the importance of the revised laws in streamlining legal interpretation and judicial processes across all levels of the legal system.

"We are here today to formally present to you, Chief Justice, these updated law volumes following the successful completion of the revision project and the President's directive that they take effect this month," said Mr. Johari.

"This will support the Judiciary in delivering justice more effectively to Tanzanian citizens."he added

The Attorney General further highlighted that, for the first time, the entire law revision project was completed using domestic financial and human resources, without relying on donor support a move that demonstrates the government's growing capacity and commitment to self-reliance in legal sector reforms.

July 5, 2025 Advertisement

TimesMajira









HABARI

# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuimarisha ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu

July 4, 2025




Na Mwandishi wetu,Timesmajira

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeahidi kuendeleza ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu Ofisi ili kuimarisha utendaji kazi na kuboresha huduma kwa wananchi.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria Bi. Neema Ringo akizungumza kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hamza Johari tarehe 4 Julai, 2025 mara baada ya kutembelea banda la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yanayofanyika katika viwanja vya Julius Nyerere Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

FULLSHANGWE blog
CONTACT:
phone: +255 713 410 676
+255 755 333 372
P.O BOX 78392, Dar es Salaam
Email. johnbukuku@gmail.com

Home Biashara Burudani Magazeti Mchanganyiko Michezo Siasa Teknolojia TV Makala

# WANANCHI WAKARIBISHWA KUTEMBELEA BANDA LA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI




Wananchi wametakiwa kufika katika banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali lililopo kwenye Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba, ili kupata huduma za kisheria na elimu kuhusu masuala mbalimbali ya sheria.

Wito huo umetolewa leo na Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Bi. Neema Ringo, wakati wa maonesho yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Bi. Ringo amesema kuwa kwa mara ya kwanza, ofisi hiyo inashiriki maonesho hayo kama taasisi huru, tofauti na miaka ya nyuma ambapo walikuwa wakishiriki kupitia banda la Mahakama Kuu ya Tanzania.

"Kwa mwaka huu tumeona ni muhimu kuwa na banda letu ili kuwa karibu zaidi na wananchi kwa kuwapatia huduma na kuwaelimisha kuhusu majukumu tunayoyatekeleza," alisema Ringo.

# MITANDAONI
## 02/07/2025

nipashetz




25

Liked by **kitomari.salome** and others

**nipashetz** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesaini hati ya makubuliano na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (LST), kwa ajili ya kushirikiana katika masuala mbalimbali yanayohusu taaluma ya Sheria.

oagtanzania



oagtanzania HABARI PICHA

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari amehudhuria sherehe za 72 za kuapishwa na kupokelewa kwa Mawakili wa Kujitegemea zilizofanyika tarehe 3 Julai, 2024 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Jiji Dodoma.

Jumla ya Mawakili 449 wameapishwa na kupokelewa na baada ya kufaulu usaili wao na kukubaliwa rasmi kuwa Mawakili.

Mgeni Rasmi katika sherehe hizo za uapisho wa Mawakili wa Kujitegemea ni Jaji Mkuu wa Tanzania Mhe. Jaji George Mcheche Masaju. less

oagtanzania




**oagtanzania** *OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KUIMARISHA USHIRIKIANO NA OFISI YA WAZIRI MKUU*

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeahidi kuendeleza ushirikiano na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuimarisha utendaji kazi na kuboresha huduma kwa wananchi.

**OAG Tanzania**

2d ·

*HABARI PICHA*

Wajumbe wa Menejimenti na baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tarehe 2 Julai, 2025 wameshiriki Mafunzo kuhusu upimaji wa Utendaji Kazi "e-Utendaji (WATUMISHI) kwa Watumishi Umma.



# MITANDAONI
01/07/2025



oagtanzania




View insights

Boost post

14 2 2

Liked by **leilamuhaji** and others

**oagtanzania** Jipatie Nakala yako kwa Mpiga Chapa wa Serikali au duka la vitabu la TPH

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz


Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania


**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora